Nuru ya Kiswahili, Juzuu 3(2), Desemba 2024: 68-97
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru32.6897

Mawanda na Mazingira ya Utokeaji wa Kirai Kihusishi katika Sentensi za Kiswahili

Elishafati J. Ndumiwe
Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Tanzania
elishandumiwe@saut.ac.tz

Ikisiri

Utambuzi na ubainishaji wa kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili unaibua mgogoro wa kimtazamo, miongoni mwa wanasarufi wa lugha hii, kuhusu mawanda na mazingira ya utokeaji wa kirai hicho. Mawanda hayo ni Kngo+H, Kngo+H+Kngo na H+Kngo. Kujiegemeza katika mawanda haya kumechagiza dosari kadhaa katika utambuzi wa kirai hiki na aina zingine za virai. Kwa hiyo, makala hii inalenga kudhihirisha mawanda na mazingira ya utokeaji wa kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili. Utafiti unaoripotiwa katika makala hii ulifanyika maktabani na uwandani. Mbinu zilizotumika kukusanya na kuchambua data ni usomaji matini kutoka Riwaya ya *Nagona* ya Kezilahabi (2011), upimaji wa usahihi wa kisarufi, na usaili. Mkabala wa Kileksika ulioasisiwa na Lewis (1993) ulitumika katika kufasiri na kuchanganua data za utafiti uliozaa makala hii. Matokeo yanaonesha kuwa mawanda ya kirai kihusishi huanzia kwenye kihusishi na hukomea katika kirai nomino cha baada yake. Vilevile, kirai hiki hutokea baada ya nomino, kitenzi, kibainishi, kivumishi, kiwakilishi, kuhusishi au kiunganishi katika sentensi za Kiswahili. Msimamo wa makala hii ni katika mawanda ya H+Kngo kwa sababu mawanda haya ndiyo yanayoakisi mawanda ya virai vingine vya Kiswahili. Kwa hiyo, usahihi wa utambuzi na ubainishaji wa kirai hiki unatoa uwezekano wa uainishaji wa viambajengo vingine vya sentensi kwa usahihi.

Dhana za Msingi: Kirai kihusishi, sentensi, mazingira, mawanda, na mkabala wa kileksika

Utangulizi

Kirai kihusishi ni mojawapo ya virai vinavyokunjiwa katika virai vingine katika sentensi za Kiswahili. Mara nyingi, kirai hiki hukunjiwa ndani ya kirai nomino au kirai kitenzi (Wesana-Chomi, 2017). Kutokana na hilo, kirai kihusishi ni mojawapo ya viambajengo vya kimuundo vyenye kutegemea kuwapo kwa viambajengo vingine katika sentensi. Kwa mujibu wa Wesana-Chomi (2017) na Ndumiwe (2021), katika lugha ya Kiswahili, kirai kihusishi kina muundo mmoja tu ambao ni kihusishi kikifuatiwa na kirai nomino (H+KN). Miundo tofauti ya kirai nomino inaweza kujitokeza katika mazingira hayo. Kwa hiyo, kihusishi ni neno kuu linalounda kirai kihusishi katika sarufi ya lugha ya Kiswahili (Matei, 2008).

Baadhi ya maandiko ya sarufi ya lugha ya Kiswahili yamesheheni dosari mbili kuhusu kirai kihusishi. Dosari ya kwanza inahusu mawanda ya kirai kihusishi katika tungo, yaani mahali kinapoanzia na kukomea. Kuhusu dosari hiyo, baadhi ya maandiko yanakinzana namna ya kuweka mawanda ya kirai kihusishi katika tungo. Mathalani, Matinde (2012) anaonesha kwamba kirai kihusishi kinaanzia kwenye kiambajengo cha kabla yake na kihusishi chenyewe (Kngo+H[1]). Kwa kuzingatia hilo, kirai kihusishi kinajengwa na viambajengo viwili, kiambajengo cha kabla na kihusishi chenyewe, katika mkururo wa viambajengo kuelekea kulia kama invyodhihirika katika Mfano Na. 1 kutoka kwa Matinde (2012:169).

(1) a. Chukua pesa zilizoko **juu ya** kabati ukanunue mboga.
b. Nyoka aliingia **ndani ya** shimo.
c. Simu tamba hazitakiwi kutumika **wakati wa** ibada.
d. Jua lilipokuwa kali, tulijibanza **chini ya** kivuli cha mti.

[1] Kirefu cha kiambajengo+kihusishi

Maneno yaliyopigiwa mistari katika Mfano Na. 1(a)-(d) yamebainishwa kama virai vihusishi katika tungo hizo. Kwa upande wa Matei (2008), kirai kihusishi kinaanzia kwenye kiambajengo cha kabla, kihusishi chenyewe, na kiambajengo cha baada ya kihusishi hicho (Kngo+H+Kngo[2]). Kwa msingi huo, kirai kihusishi kinajengwa na viambajengo vitatu, yaani kiambajengo cha kabla, kihusishi chenyewe na kiambajengo cha baada katika mkururo wa viambajengo vinavyofuatana kuelekea kulia. Katika kuthibitisha hilo, Mfano Na. 2 kutoka kwa Matei (2008) unaweza kurejelewa.

(2) a. Huenda tukahitaji kuishi **nje ya kijiji**.
b. Koo hizi ziliishi **karibu na mpaka**.
c. Saa imetundikwa **juu ya ukuta**.
d. Nguo zimo **ndani ya sanduku**.
Chanzo: Matei (2008:205-206)

Maneno yaliyopigiwa mistari katika Mfano Na. 2 yamebainishwa kama virai vihusishi katika tungo hizo. Naye Wesana-Chomi (2017) anaonesha kwamba kirai kihusishi katika lugha ya Kiswahili kinaanzia kwenye kihusishi kikifuatiwa na kiambajengo cha baada yake (H+Kngo[3]). Kwa msingi huo, kirai kihusishi kinajengwa na viambajengo viwili, yaani kihusishi chenyewe kikifuatiwa na kiambajengo kingine katika mkururo unaoelekea kulia. Mfano Na. 3 kutoka kwa Wesana-Chomi (2017) umerejelewa ili kuthibitisha maelezo hayo.

(3) a. Sheria **ya ndoa ya mwaka 1971**.
b. Nilisafiri **mpaka Dodoma**.
c. Alifungwa **kwa sababu halali**.
d. Nimekuja **kwa ajili ya mkutano**.
Chanzo: Wesana-Chomi (2017:120-124)

[2] Kirefu cha kiambajengo+kihusishi+kihusishi
[3] Kirefu cha kihusishi+kiambajengo

Katika Mfano Na. 3, viambajengo vilivyopigiwa mistari vimebainishwa kama virai vihusishi katika tungo hizo. Mkanganyiko huu wa kiubainishaji unaweza kusababisha dosari zingine katika utambuzi wa viambajengo vingine vinavyotangulia au kufuatana na kirai kihusishi katika tungo. Dosari hii ya kwanza inaonesha kuwa kirai kihusishi kimebainishwa kwa namna tatu tofauti. Namna ya kwanza inahusisha viambajengo viwili, yaani kiambajengo cha kabla yake na kihusishi (Kngo+H). Namna ya pili inahusisha viambajengo vitatu, yaani kiambajengo cha kabla, kihusishi, na kiambajengo cha baada yake (Kngo+H+Kngo). Namna ya mwisho inahusisha viambajengo viwili, yaani kihusishi na kiambajengo cha baada yake (H+Kngo).

Dosari ya pili inayojitokeza katika maandiko ya wanasarufi tangulizi inahusu uwekwaji wa kirai kihusishi katika kundi la kirai kivumishi, kirai kielezi, au kirai kiunganishi. Dosari hii inatokana na kutokutambuliwa kwa kirai kihusishi katika maandiko hayo au mifano ya kirai kihusishi kutajwa katika aina zingine za virai kama vile kirai kiunganishi au kirai kivumishi. Kwa mfano, Massamba na wenzake (2012) na Saluhaya (2016) wamevitaja virai vifuatavyo kama virai viunganishi.

(4) a. kwa baba yake
b. kwa mguu
c. kwa kijiko
d. kwa amri ya jeshi

Chanzo: Massamba na wenzake (2012:118)

(5) a. kwa amri ya jeshi
b. katika chumba
c. kwenye pombe
d. kwa baba yake

Chanzo: Saluhaya (2016:125)

Katika Mfano Na. 4(a)-(d) na 5(a)-(d), virai hivyo vimebainishwa kama viunganishi. Sanjari na hayo, mifano tajwa inaendana na miundo ya virai vihusishi katika tungo zilizopo katika Mfano Na. 3(a)-(d). Katika maandiko ya Massamba na wenzake (2012) na Saluhaya (2016), kirai kihusihi

hakijatajwa kama mojawapo ya virai vilivyopo katika lugha ya Kiswahili. Kwa mtazamo wa mwandishi wa makala hii, virai vilivyopo katika Mfano Na. 4 na 5 ni virai vihusishi wala siyo virai viunganishi. Aidha, baadhi ya mifano katika maandiko kadhaa imekibainisha kirai kihusishi kama kirai kivumishi. Mfano wa maandiko hayo ni Matinde (2012) na Massamba na wenzake (2012). Mifano ifuatayo inadhihirisha maelezo haya.

(6) a. Kilimo **cha umwagiliaji**
b. Mzee **mwenye duka kubwa**
c. –**enye kelele nyingi**
d. –**enye kuumwa kichwa**
Chanzo: Massamba na wenzake (2012:110-111)

(7) a. Mti **wenye** **matunda**
b. Mwanafunzi **mwenye hasira**
c. Baniani **mwenye duka**
d. Mteja **mwenye gari kubwa**
Chanzo: Matinde (2012:167)

Viambajengo vilivyopigiwa mistari vimebainishwa kama virai vivumishi katika maandiko tajwa. Pamoja na hilo, mifano hiyo inaendana na miundo ya virai vihusishi iliyopo katika Mfano Na. 3(a)-(d). Mifano hiyo inaangukia katika kirai kihusishi badala ya kirai kivumishi kama ilivyobainishwa katika maandiko ya Massamba na wenzake (2012) na Matinde (2012). Vilevile, baadhi ya mifano katika maandiko ya wanasarufi tangulizi inaingizwa katika kundi la kirai kielezi badala ya kirai kihusishi. Mathalani, Massamba na wenzake (2012) wameweka mifano ifuatayo katika kundi la kirai kielezi.

(8) a. mara nyingine
b. kwa sababu amefanya bidii
c. kwa haraka
d. hivi karibuni
Chanzo: Massamba na wenzake (2012:116)

Virai katika Mfano Na. 8 vimetambulishwa na Massamba na wenzake (2012) kama virai vielezi. Hata hivyo, miundo yake inafanana na miundo iliyobainishwa katika katika Mfano Na. 3 data kuhusu mawanda ya kirai kihusishi (H+kngo). Katika andiko la Massamba na wenzake (2012), kirai kihusihi hakijatajwa kama mojawapo ya virai vilivyopo katika lugha ya Kiswahili.

Pamoja na dosari tajwa, maandiko yaliyorejelewa katika sehemu iliyotanguliwa ndiyo hutumika katika ufundishaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili (hasa sintaksia) katika shule za sekondari na vyuoni. Suala hili limesababisha dosari nyingi za uainishaji wa maneno, virai na uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi katika ngazi tofauti za elimu. Ingawa tafiti au maandiko kadhaa yameshughulikia suala hili, kirai kihusishi hakijaelezwa kwa usahihi. Maelezo yaliyomo katika maandiko mengi ya sarufi ya Kiswahili yanaleta mkanganyiko wa kuainisha na kubainisha mawanda ya kirai kihusishi katika tungo za Kiswahili. Vilevile, maelezo katika maandiko yaliyorejelewa hukitaja kirai kihusishi kama kirai kivumishi (rejea Mfano Na. 7 kutoka kwa Matinde, 2012), kirai kielezi (rejea Mfano Na. 8 kutoka kwa Massamba na wenzake, 2012) au kirai kiunganishi (rejea Mfano Na. 5 kutoka kwa Saluhaya, 2016). Kwa hiyo, makala hii inatarajia kuondoa mkanganyiko wa kubainisha na kuainisha kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili. Vilevile, yanatarajiwa kusaidia kutokichanganya na virai vingine kwa kuonesha mazingira ya utokeaji wa kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili.

Kiunzi cha Nadharia

Uchanganuzi wa data ulitumia Mkabala wa Kileskika ulioasisiwa na Lewis (1993). Mkabala huu unaonesha kuwa lugha huundwa kwa muunganiko wa

viambajengo vinavyozalisha usemi katika lugha husika. Kwa mujibu wa Lewis (1993), mkabala huu una misingi mitatu. Msingi wa kwanza ni mfuatano wa viambajengo vya kimuundo katika tungo. Kwa kuzingatia msingi huu, viambajengo vya kimuundo hushirikiana na viambajengo vingine katika kuzalisha tungo. Msingi wa pili ni uwakilishi wa kisintaksia katika muundo wa nje. Kuhusu msingi huu, uchanganuzi wa data kwa kutumia Mkabala wa Kileksika hautambui kuwapo kwa muundo wa ndani wa tungo. Tungo huchanganuliwa kwa namna inavyojidhihirisha katika usemaji wa lugha husika, yaani muundo wa nje. Msingi wa tatu ni uchanganuzi wa viambajengo vya tungo katika mchoroti, yaani mti matawi. Kwa kuzingatia msingi huu, Mkabala wa Kileksika hushughulikia uchanganuzi wa viambajengo vya kimuundo katika michoroti. Uchanganuzi na ufasiri wa data za utafiti unaoripotiwa katika makala hii umetumia msingi wa kwanza na wa tatu. Msingi wa kwanza umetumika kufasiri viambajengo vinavyotokea kabla ya kirai kihusishi katika mkururo wa viambajengo unaoanzia kushoto kuelekea kulia. Kwa kuzingatia msingi huu, makala inaonesha kirai kihusishi kinavyotokea kwa kufuatana na viambajengo vingine vya kimuundo katika sentensi za Kiswahili. Msingi wa tatu umetumika kuchanganua viambajengo vinavyotokea pamoja na kirai kihusishi katika tungo za Kiswahili katika michoroti.

Methodolojia

Utafiti unaoripotiwa katika makala hii ulifanyika maktabani na uwandani. Kwa upande wa maktabani, mtafiti alikusanya tungo zenye virai vihusishi kutoka Riwaya ya *Nagona* iliyoandikwa na Kezilahabi (2011). Riwaya hii iliteuliwa kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza, imeandikwa na mwandishi ambaye ni mtaalamu na mzawa wa lugha ya Kiswahili. Isitoshe, riwaya hii hutumika katika ngazi tofauti za elimu. Kwa kuzingatia hayo, Kiswahili

kilichotumika ni sanifu. Sababu ya pili, riwaya teule ina masimulizi ya kinathari yenye tungo fupifupi ambazo zinaonesha kuwapo kwa virai vihusishi vingi. Kwa hiyo, riwaya hii iliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Matini iliyolengwa ni ile yenye matumizi makubwa ya virai vihusishi. Riwaya ya *Nagona* (Kezilahabi, 2011) ilikidhi kigezo hiki. Aidha, andiko hilo liliwakilisha vyanzo vingine vya data ambamo data za makala zingeliweza kupatikana.

Kwa upande wa uwandani, utafiti unaoripotiwa katika makala hii ulitumia watoataarifa kumi (10): wanne (wahadhiri wa sintaksia katika vyuo kikuu vinne, yaani kila chuo mhadhiri mmoja) na sita (wanafunzi wa sintaksia ya Kiswahili kutoka Chuo cha SAUT-Mwanza). Wahadhiri wanne walisailiwa kuhusu muundo, mawanda na mazingira ya utokeaji wa virai vihusishi vilivyokusanywa kutoka kwenye teule. Wanafunzi wa sita wa sintaksia ya Kiswahili kutoka chuo cha SAUT walishiriki katika upimaji wa usahihi wa kisarufi wa tungo zilizokusanywa kutoka riwaya teule.

Mbinu zilizotumika kukusanya data kutoka riwaya teule ni uchambuzi matini, upimaji wa usahihi wa kisarufi, na usaili. Mbinu ya uchambuzi matini ilitumika kwa sababu data zilikusanywa kutoka katika matini andishi. Mtafiti alisoma na kuchambua matini teule kwa makini, huku akibainisha tungo zenye virai vihusishi na kuzinukuu katika daftari. Baada ya shughuli hiyo, mtafiti aliwapatia wanafunzi sita wa sintaksia ya Kiswahili kuhakiki usahihi wa kisarufi wa tungo hizo. Tungo zilizobaininika kuwa na makosa ya kisarufi ziliondolewa. Aidha, tungo zilizobainika kuwa sahihi zilichukuliwa kwa ajili ya usaili na wahadhiri wa sintaksia. Shughuli ya uhakiki ilifuatiwa na shughuli ya uchambuzi wa tungo zenye usahihi wa kisarufi. Katika shughuli hiyo, mtafiti aliwasili

wahadhiri wanne wa sintaksia ya Kiswahii kutoka vyuo vikuu vinne kwa kuzingatia vipengele vya muundo, mawanda, na mazingira ya utokeaji wa KH katika lugha ya Kiswahili. Tungo zenye muundo, mawanda, na mazingira ya utokeaji wa KH yanayofanana ziliwekwa katika kundi moja. Mifano ya tungo zilizopatikana katika kila kundi ilichukuliwa na kuwekwa katika kipengele cha matokeo ya utafiti.

Uchambuzi wa data ulitumia mkabala wa kitaamuli. Katika mkabala huu, kuna mbinu tofauti kutegemeana na data za utafiti (Angouri, 2010). Data za utafiti huu ni masimulizi, yaani riwaya. Mbinu za uchambuzi wa data za aina hii ni mbili, yaani uchambuzi wa vijenzi vya riwaya na uchambuzi wa dhima ya riwaya (Gimenez, 2010). Utafiti unaoripotiwa katika makala hii ulitumia mbinu ya uchambuzi wa vijenzi vya riwaya. Gimenez (2010) anaeleza kuwa uchambuzi wa vijenzi vya riwaya huangalia sentensi na mpangilio wake katika simulizi husika. Aidha, uwasilishaji wa data kwa kuzingatia mkabala wa kitaamuli hutumia mbinu mbalimbali (Angouri, 2010). Utafiti unaoripotiwa katika makala hii ulitumia mbinu ya maelezo na vielelezo. Mtafiti ametoa ufafanuzi kuhusu mazingira ya utokeaji wa kirai kihusishi katika tungo za Kiswahili. Baada ya maelezo hayo, mtafiti ameonesha vielelezo vya uchanganuzi wa tungo na kuonesha mazingira hayo katika michoroti.

Mawanda ya Kirai Kihusishi katika Kiswahili

Utafiti ulibaini kuwa kirai kihusishi katika lugha ya Kiswahili kinaanzia kwenye kihusishi chenyewe kuelekea kulia mpaka kirai nomino kinachotokea baada yake kinapoishia. Kwa msingi huo, mawanda ya kirai kihusishi yanaanzia kwenye kihusishi na yanaishia kwenye kirai nomino

kinachotokea baada ya kihusishi hicho. Data Na. 1 inaweza kurejelewa ili kuthibitisha maelezo hayo.

(1) a. Mawazo yangu yalivutiwa **na** *mlio wa paka kutoka pembe moja ya nyumba* (uk. 4).
b. Niliona makazi yanayofanana **na** *mji mdogo* (uk. 2).
c. Alitembea kuelekea **kwenye** *lango la dhahabu* (uk. 52).
d. Lango **la** *chuma cha pua* lilifunguka (uk. 61).
e. Maua **ya** *bustani hii* yalikuwa meupe na yalitoa mwanga (uk. 22).
f. Mkombozi **wa** *kwanza* alisulubiwa (uk. 22).
Chanzo: *Nagona* (2011)

Katika Data Na. 1(a)-(f), viambajengo vilivyopigiwa mistari ni virai vihusishi. Virai hivyo vinaanzia kwenye vihusishi ambavyo vimebainishwa kwa kukozwa katika Data Na. 1(a)-(f). Aidha, virai hivyo vinaishia kwenye kirai nomino ambacho kimebainishwa kuwekewa hatimlazo katika Data Na. 1(a)-(f). Virai vihusihi ni tegemezi katika viambajengo vingine vya sentensi kwa sababu hutokea kwa kukunjiwa ndani ya viambajengo vingine. Mathalani, katika Data Na. 1(a)-(c), virai vihusishi vimekunjiwa katika kirai kitenzi. Vilevile, katika Data Na. 1(d)-(f), virai vihusishi vimekunjiwa katika kirai nomino. Kwa kutumia Mkabala wa Kileksika wa Lewis (1993), mawanda ya kirai kihusishi katika lugha ya Kiswahili yanaweza kubainishwa kwa kuzingatia msingi wa mfuatano wa viambajengo vya kimuundo. Kwa hiyo, kimuundo, kirai nomino hutokea baada ya kihusishi na vyote kwa pamoja hujenga kirai kihusishi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1[4].

Kielelezo Na. 1: Mawanda ya Kirai Kihusishi katika Kiswahili

[4] Katika makala hii, vielelezo vilivyotumika vinaonyesha uchanganuzi wa KH tu kwa sababu ya lengo la makala hii. Hata hivyo, kila kirai kihusihi kilichochanganuliwa ni sehemu ya sentensi ambazo zimebainishwa kabla ya kielelezo husika.



a. **na** mlio wa paka kutoka pembe moja ya nyumba
b **na** mji mdogo
c. **kwenye** lango la dhahabu
d. **la** chuma cha pua
e. **ya** bustani hii
f. **wa** kwanza

Kielelezo Na. 1 kinaonesha mawanda ya kirai kihusishi katika lugha ya Kiswahili. Katika mawanda haya, kirai kihusishi kinajengwa na viambajengo umbu viwili, yaani kihusishi chenyewe na kirai nomino. Ndani ya kirai nomino kunaweza kuwa na virai vingine ndani yake. Alama ya pembetatu katika Kielelezo Na. 1 inaonesha kuwa kiambajengo hicho kinaweza kuchanganuliwa zaidi. Sambamba na matokeo haya, utafiti wa Gitonga & Nandelenga (2022) katika lugha ya Kiigembe umeonesha kuwapo kwa miundo minne ya kirai kihusishi katika lugha hiyo: (a) kihusishi na kirai nomino (H+KN), (b) kihusishi, kihusishi na kirai nomino (H+H+KN), (c) kihusishi na kitenzijina na (d) kihusishi na kirai kielezi (H+KE). Miundo hiyo huanzia kwenye chenyewe kuelekea kulia. Kulingana na matokeo ya utafiti huu, muundo wa H+KN ndio hujitokeza katika lugha ya Kiswahili miongoni mwa miundo iliyotajwa kuwapo katika lugha Kiigembe kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1.

Mazingira ya Utokeaji wa Kirai Kihusishi

Utafiti unaoripotiwa katika makala hii umebainisha kuwapo kwa mazingira tofauti ya utokeaji wa kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili. Mazingira hayo hutokana na mfuatano wa maneno katika sentensi hizo.

Kirai hiki hutokea kwa kutegemea uwapo wa viambajengo vingine katika sentensi, yaani hukunjiwa katika viambajengo tofauti. Kwa mantiki hiyo, kirai kihusishi ni miongoni mwa virai vidogovidogo vinavyotegemea kuwapo kwa virai vingine katika tungo. Aidha, yapo mazingira ambayo kirai hiki huweza kuondolewa bila kuathiri maana ya msingi ya tungo. Katika utafiti unaoripotiwa katika makala hii, imebainika kuwa kirai kihusishi hutokea baada ya nomino, kitenzi, kibainishi, kivumishi, kielezi, kihusishi na kiunganishi.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya nomino

Kutokana na utafiti unaoripotiwa katika makala hii, mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili huruhusu kirai kihusishi kutokea baada ya nomino. Katika mazingira haya, kirai kihusishi hukunjiwa ndani ya kirai nomino cha kabla ya kitenzi au kirai nomino cha baada ya kitenzi (Gitonga & Nandelenga, 2022). Mifano katika Data Na. 2 inaonesha utokeaji wa kirai kihusishi baada ya nomino katika sentensi za Kiswahili.

(2) a. W**atu** kama hao huwa hawasikilizwi (uk. 29).
N KH
b. **Lango** la chuma cha pua lilifunguka (uk. 61).
N KH
c. **Nyuma** ya nyumba hizi palitokea nyumba mbovu zaidi (uk. 2).
N KH
d. Sijawaona **waongo** kama ninyi (uk. 62).
N KH
e. Walifika kutafuta **mawaidha** kuhusu migogoro yao (uk. 15).
N KH
f. Nilisikia **vicheko** vya watu (uk. 1)
N KH
Chanzo: *Nagona* (2011)

Viambajengo vilivyopigiwa mistari katika Data Na. 2(a)-(g) ni virai vihusishi vilivyotokea baada ya nomino. Baadhi ya virai hivyo vimetokea

baada ya nomino ya kabla ya kitenzi kama ilivyo katika Data Na. 2(a)–(c). Virai vihusishi vingine hutokea baada ya nomino iliyopo katika kirai kitenzi kama ilivyo katika Data Na. 2(d)-(f). Kwa hiyo, kirai kihusishi hutokea baada ya nomino iliyomo katika sentensi. Katika mazingira haya, kirai kihusishi ni kijenzi cha kirai nomino. Wesana-Chomi (2017) na Ndumiwe (2020) wameonesha kuwa nomino na kirai kihusishi ni muundo mmojawapo wa kirai nomino cha Kiswahili. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika wa Lewis (1993), viambajengo vya kimuundo hubainishwa kutokana na mfuatano wake na viambajengo vingine vya kimuundo kama inavyodhihirika katika Kielelezo Na. 2.

Kielelezo Na. 2: Kirai Kihusishi baada ya Nomino katika Tungo za Kiswahili



a. watu	**kama**	hao
b. lango	**la**	chuma cha pua
c. nyuma	**ya**	nyumba hizi
d. waongo	**kama**	ninyi
e. mawaidha	**kuhusu**	migogoro yao
f. vicheko	**vya**	watu

Katika Kielelezo Na. 2, imebainika kuwa kirai kihusishi katika tungo za Kiswahili kimetokea kwa kufuatana na nomino kama ilivyo katika Data Na. 2. Katika mazingira haya, kirai hiki hukunjiwa katika nomino na vyote kwa pamoja huunda kirai nomino chenye nomino na kirai kihusishi. Aidha, baada ya kihusishi, kuna kirai nomino kinachotokea baada yake na hutokea

kama kiambajengo umbu cha kirai kihusishi. Kirai nomino kinachotokea kama kiambajengo umbu cha kuhusishi huwa katika miundo tofautitofauti. Mathalani, katika Data Na. 2(a) na (d), kirai nomino kimeundwa na kiwakilishi.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kitenzi kikuu

Utafiti unaoripotiwa katika makala hii umebaini kuwa kirai kihusishi cha Kiswahili kutokea baada ya kitenzi kikuu. Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kitenzi kikuu hutokana na kuwapo kwa kitenzi sielekezi katika muundo wa sentensi. Kwa mujibu wa Wesana-Chomi (2017), kirai kihusishi kinachotokea baada ya kitenzi huwa kiambajengo cha hiari cha kirai kitenzi. Kutokana na hilo, kirai hicho kinaweza kuondolewa katika sentensi bila kuathiri maana ya msingi ya sentensi. Kwa msingi huo, kirai kihusishi cha baada ya kitenzi hukumusha taarifa inayotolewa na kitenzi. Data Na. 3 inaonesha utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kitenzi katika sentensi za Kiswahili.

(3) a. Kizee **kiliturudisha** kwenye njia tuliyotoka (uk. 34).
T KH
b. Mto huu **utakapofurika** hadi mjini (uk. 12).
T KH
c. **Hukusamehewa** hata dhambi moja (uk. 28).
T KH
d. Kamasi lilianza **kujitingisha** kama funza lililopata joto (uk. 27).
T KH
e. **Wapelekeeni** kwenye bonde la mauti (uk. 53).
T KH
f. Safari hii **nilijibu** bila kukawia (uk. 55).
T KH
g. **Uliungama** kwa padri mlevi (uk. 29).
T KH
Chanzo: *Nagona* (2011)

Viambajengo vilivyopigiwa mistari katika Data Na. 3(a)-(g) ni virai vihusishi vilivyotokea baada ya kitenzi kikuu. Kitenzi hicho hakina nomino inayotokea baada ya kitenzi husika. Sambamba na matokeo hayo, Wahome (2024) anaeleza kuwa kirai kihusishi hufanya kazi kama kielezi kwa kutokea baada ya kitenzi. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, viambajengo vya kimuundo hutokea kwa kufuatana na viambajengo vingine vya kimuundo kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 3.

Kielelezo Na. 3: Kirai Kihusishi baada ya Kitenzi katika Tungo za Kiswahili



a. kiliturudisha	**kwenye**	njia tuliyotoka
b. utakapofurika	**hadi**	mjini
c. hukusamehewa	**hata**	dhambi moja
d. kujitingisha	**kama**	funza lililopata joto
e. wapelekeni	**kwenye**	bonde la mauti
f. nilijibu	**bila**	kukawia
g. uliungama	**kwa**	padri mlevi

Kwa kurejelea katika Kielelezo Na. 3, kirai kihusishi kimetokea baada ya kitenzi kikuu katika tungo hizo. Utafiti ulibaini kuwa kuna kirai nomino baada ya kihusishi kinachosimama kama kiambajengo umbu cha kirai kihusishi. Kwa hiyo, kihusishi na kirai nomino kilichokunjiwa ndani KH hujenga kirai kihusishi. Hii inamaanisha kuwa ndani ya KH kuna kirai nomino kinachotokea baada ya kihusishi.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kibainishi

Katika lugha ya Kiswahili, kibainishi[5] hutokea kwa kuambatana na nomino au kiwakilishi cha nomino (Philipo, 2017; Champunga, 2019; Ndumiwe, 2020). Kimsingi, kibainishi ni neno ambalo hutumika pamoja na nomino au kiwakilishi kudhihirisha umahususi wa nomino au kiwakilishi (Philipo, 2017). Ufafanuzi huu hutofautiana na ule wa kivumishi ambao huonyesha kuwa kivumishi ni neno linaloonyesha sifa kuhusu nomino au kiwakilishi. Kutokana na utafiti uliozaa makala hii, kirai kihusishi cha Kiswahili hutokea baada ya kibainishi. Utokeaji wa kirai hiki katika mazingira tajwa hutokana na ukumushaji wa taarifa iliyopo kabla yake. Katika mazingira haya, kirai kihusishi huwa kiambajengo cha hiari kwa sababu kinaweza kuondolewa katika sentensi bila kuathiri maana ya msingi ya sentensi. Pamoja na hayo, kirai kivumishi huweza kutokea katika mazingira ya namna hii. Kutokana na hilo, ndipo Massamba na wenzake (2012) waliainisha kirai kihusishi kama kirai kivumishi. Data Na. 4 inaonesha utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kibainishi katika sentensi za Kiswahili.

(4) a. Alitikisha kichwa **chake** <u>kama alama ya kukataa</u> kuzungumza (uk. 6).
B KH
b. … akitazama katikati ya viganja **vyake** <u>kwa umakini</u> (uk. 23).
B KH
c. Nilijihisi vumbi linaingia machoni **mwangu** <u>kama dawa kali</u> (uk. 23).
B KH

---

[5] Katika sarufi ya lugha ya Kiswahili, upo mvutano miongoni mwa wanasarufi kuhusu maneno yapi yanaingia kwenye kundi la kibainishi na kivumishi. Mvutano huu umesababishwa na kuibuka kwa kategoria inayoitwa *kibainishi* ambayo hutokea kwa kuambatana na nomino au kiwakilishi kama ilivyo kwa *kivumishi*. Baadhi ya maneno yaliyoainishwa kama kivumishi yameainishwa upya kama kibainishi. Uainishaji huo umezingatia kigezo cha kidhima (Philipo, 2017; Champunga, 2019). Kwa kuwa lengo la makala hii siyo kushughulikia mvutano huo, tunaafikiana na mtazamo wa Philipo (2017) na Champunga (2019) kuhusu kuwapo kwa kibainishi na kivumishi kwa kigezo cha kidhima. Hata hivyo, kibainishi cha baada ya nomino au kiwakilishi hutokea mazingira sawa na kivumishi. Msomaji wetu anaweza kurejela maandiko tajwa kwa ajili ya kuzipambanua dhana hizo.

d. Vijana **watatu** wenye mikuki walikuwa wamekizunguka (uk. 62).
B KH

e. Wengine walikuwa njiani **mwangu** kuhusu wanawake (uk. 87).
B KH

Chanzo: *Nagona* (2011)

Katika Data Na. 4 (a)-(e), viambajengo vilivyopigiwa mistari ni virai vihusishi vinavyotokea baada ya kibainishi. Matokeo ya utafiti yanayoripotiwa katika makala hii yanaonyesha kuwa kirai kihusishi hutokea baada ya kibainishi kimilikishi au kibainishi cha namba. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, ubainishaji wa kategoria za kimuundo katika lugha mbalimbali hutegemea mfuatano wa kategoria husika na kategoria zingine katika sentensi. Kutokana na hilo, kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili hutokea kwa kutanguliwa na kibainishi kama inavyodhirika katika Kielelezo Na. 4.

Kielelezo Na. 4: Kirai Kihusishi baada ya Kibainishi katika Tungo za Kiswahili



a. chake	**kama**	alama ya kukataa
b. vyake	**kwa**	umakini
c. mwangu	**kama**	dawa kali
d. watatu	**wenye**	mikuki
e. mwangu	**kuhusu**	wanawake

Katika Kielelezo Na. 4, kirai kihusishi kimetokea baaada ya kibainishi na vyote kwa pamoja hujenga kirai kibainishi. Kutokana na hilo, ndiyo maana

Gitonga & Nandelenga (2022) wanaeleza kuwa kuna uwezekano wa kirai kihusishi kutokea baada ya kibainishi katika lugha ya Kiigembe na lugha nyingine za Kibantu. Mazingira hayo yanadhihirika pia katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu maneno yaliyotajwa kama vibainishi huonyesha umahususi wa nomino siyo sifa ya nomino.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kivumishi

Katika lugha ya Kiswahili, kivumishi hutokea kwa kufuatana na nomino au kiwakilishi (Rubanza, 2003; Khamis & Kiango, 2012; Kihore & wenzake, 2012). Matokeo ya utafiti yanayoripotiwa katika makala hii yanaonesha kuwa nomino au kiwakilishi hicho kinaweza kutokea baada ya kitenzi au kabla ya kitenzi. Utafiti uliozaa makala hii umebaini kirai kihusishi hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi kilichotokea kabla ya kivumishi. Data Na. 5 inaonesha virai vihusishi vilivyotokea baada ya kivumishi katika sentensi za Kiswahili.

(5) a. Nyimbo **nzuri** za ndege wa asubuhi ziliburudisha … (uk. 95).
V KH
b. Palitokea shimo **kubwa** kwenye kitovu cha duara (uk. 102).
V KH
c. Nchi **nyingi** katika ulimwengu wa tatu zilipata pigo (uk. 31).
V KH
d. …ilikuwa ikilindwa na askari **mkondefu** mwenye bunduki (uk. 37).
V KH
e. …palikuwa na maua **mazuri** yenye rihi ya kupendeza (uk. 32).
V KH
f. Sijapata kuona usiku **mrefu** kama huo (uk. 83).
V KH

Chanzo: *Nagona* (2011)

Katika Data Na. 5(a)-(f), viambajengo vilivyopigiwa mistari ni virai vihusishi vilivyotokea baada ya kivumishi katika sentensi za Kiswahili. Katika mifano tajwa, virai vihusishi vimetokea upande wa kirai nomino cha

kabla ya kitenzi au kirai nomino cha baada ya kitenzi kutegemeana na mazingira ya nomino inayokumushwa katika sentensi. Mathalani, katika Data Na. 5(a)-(c), virai vihusishi vimetokea ndani ya kirai nomino cha kabla ya kitenzi, ilhali katika Data Na. 5(d)-(f) virai vihusishi vimetokea ndani ya kirai nomino cha kabla ya kitenzi. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, utokeaji wa viambajengo vya kimuundo katika lugha mbalimbali hutegemea mfuatano wake na viambajengo vingine katika tungo. Kwa hiyo, kulingana na msingi wa kiunzi hiki cha kinadharia, kirai kihusishi hutokea kwa utegemezi wa kufuatana na kivumishi katika sentensi za Kiswahili kama inavyodhihirika katika Kielelezo Na. 5.

Kielelezo Na. 5: Kirai Kihusishi baada ya Kivumishi katika Tungo za Kiswahili



a. nzuri	**za**	ndege wa asubuhi
b. kubwa	**kwenye**	kitovu cha duara
c. nyingi	**katika**	ulimwengu wa tatu
d. mkondefu	**mwenye**	bunduki
e. mazuri	**yenye**	rihi ya kupendeza
f. mrefu	**kama**	huo

Kielelezo Na. 5 kinaonyesha kirai kihusishi kinachotokea baada ya kivumishi katika tungo za Kiswahili. Aidha, kivumishi na kirai kihusishi, kwa pamoja, ndivyo huunda kirai kivumishi. Kulingana na Ilori (2015), kirai kihusishi katika lugha za Kibantu (Kigala) huweza kutokea kwa

kufuatana na viambajengo mbalimbali vya kimuundo. Kwa hiyo, katika lugha ya Kiswahili imebainika kuwa kirai kihusishi hutokea baada ya kivumishi kama ilivyo katika Kielelezo Na. 5.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kiwakilishi

Kiwakilishi husimama badala ya nomino ambayo haipo dhahiri katika sentensi (Kihore na wenzake, 2012). Mazingira ambayo kiwakilishi hutokea huruhusu nomino yoyote yenye kuendana na muktadha wa sentensi kutokea (Rubanza, 2003). Ilibainika kwamba kirai kihusishi hutokea baada ya kiwakilishi kilichopo kabla ya kitenzi au baada ya kitenzi. Kwa hiyo, kirai kihusishi cha baada ya kiwakilishi hutoa maelezo zaidi kuhusu kiwakilishi husika. Mifano katika Data Na. 6 inathibitisha utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kiwakilishi katika sentensi za Kiswahili.

(6) a. **Vile** vya chini vilikuwa vimeanza kuliwa na mchwa (uk. 4).
W KH
b. Sisi ni miongoni mwa **wale** wenye bahati (uk. 96).
W KH
c. Milio ya ndege ilisikia **hapa** na pale (uk. 2).
W KH
d. Tulimfuata **yeye** hadi penye duara (uk. 53).
W KH
e. kwa mbali kidogo tulimwona **yule** wa kwanza (uk. 82).
W KH
Chanzo: *Nagona* (2011)

Virai vihusishi katika mifano iliyopo katika Data Na. 6(a)-(e) vimepigiwa mistari. Virai hivyo vimetokea baada ya kiwakilishi katika tungo hizo. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, utokeaji wa kategoria za kimuundo hutokana na mfuatano na kategoria zingine. Kwa hiyo, kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili hutokea kwa kutanguliwa na kiwakilishi cha kabla au baada ya kitenzi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 6.

Kielelezo Na. 6: Kirai Kihusishi baada ya Kiwakilishi katika Tungo za Kiswahili



a. vile	**vya**	chini
b. wale	**wenye**	bahati
c. hapa	**na**	pale
d. yeye	**hadi**	ndani
e. yule	**wa**	kwanza

Kielelezo Na. 6 kinaporejelewa, inabainika kuwa kirai kihusishi kimetokea baada ya kiwakilishi. Aidha, viambajengo hivi (kirai kihusishi na kiwakilishi) vinapoungana, huunda kirai nomino. Pia, baada ya kihusishi, kuna kirai nomino kinachotokea. Matokeo haya yanathibitisha maelezo ya Wesana-Chomi (2017) anayeleza kuwa ndani ya kirai nomino panaweza kukunjiwa aina zingine za virai. Utafiti uliozaa makala hii ulibaini kuwa ndani ya kirai nomino chenye muundo wa kiwakilishi, kuna kirai kihusishi kinajitokeza.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kiunganishi

Katika sentensi za Kiswahili, kiunganishi kina dhima ya kuunganisha neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi au sentensi na sentensi (Mgullu, 1999; Matei, 2008; Kihore, 2008). Katika utafiti uliozaa makala hii, ilibainika kuwa kirai kihusishi hutokea baada ya kiunganishi kinachounganisha neno na neno. Isitoshe, kirai kihusishi hutokea baada ya kiunganishi huru ‘na, au/lakini’ miongoni mwa viunganishi vinavyotajwa

kuwapo katika lugha ya Kiswahili. Utokeaji wa kirai kihusishi katika mazingira haya hutokana na udondoshaji wa nomino ileile baada ya kiunganishi. Udondoshaji hufanyika kwa lengo la kuondoa uradidi wa nomino ileile katika sentensi. Kirai kihusishi hutokea baada ya kiunganishi cha kabla au cha baada ya kitenzi katika sentensi za Kiswahili. Mifano katika Data Na. 7 inadhihirisha haya.

(7) a. … tuliona kizee kifupi kikongwe **na** chenye mapengo (uk. 32).
U KH

b. Mmoja ni wangu na wa pili ni wako (uk. 43).
U KH

c. …aliwataka wacheze mchezo wa tatu **na** wa mwisho (uk. 60).
U KH

d. Nyota yako ninaiona **lakini** kwa mbali (uk. 73).
U KH

e. Yeye alikuwa wa kwanza **au** wa mwisho (uk. 84).
U KH

Chanzo: *Nagona* (2011)

Viambajengo vilivyopigiwa mistari katika mifano iliyopo katika Data Na. 7(a)-(e) ni virai vihusishi vilivyotokea baada ya kiunganishi. Tofauti na mazingira mengine ya utokeaji wa kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili, utafiti uliozaa makala hii umebaini kuwa kirai kihusishi kilichotokea baada ya kiunganishi ni kiambajengo cha lazima kuwapo katika sentensi za Kiswahili. Kirai kihusishi cha baada ya kiunganishi kinapoondolewa katika sentensi huweza kuathiri maana ya msingi ya sentensi husika. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, utokeaji wa kategoria za kimuundo katika lugha mbalimbali hutokana na mfuatano na kategoria zingine katika sentensi. Kwa hiyo, katika sentensi za Kiswahili, kirai kihusishi hutokea baada ya kiunganishi kama inavyodhihirika katika Kielelezo Na. 7.

Kielelezo Na. 7: Kirai Kihusishi baada ya Kiunganishi katika Tungo za Kiswahili



Katika Kielelezo Na. 7, imedhihirika kuwa kirai kihusishi kimetokea baada ya kiunganishi. Viambajengo hivi, kiunganishi na kirai kihusishi, huungana kuunda kirai kiunganishi. Kulingana na matokeo ya utafiti uliozaa makala hii, kirai hiki hutokea baada ya kiunganishi kinachounganisha neno na neno, na siyo kirai na kirai au sentensi na sentensi. Matokeo haya yanaenda sambamba na utafiti wa Mathonsi (2001) katika lugha ya Kizulu aliyebaini kuwa kirai kihusishi hakiwezi kutokea baada ya kiunganishi cha sentensi kwa sababu hutokea katika mazingira ambayo kuna udondoshaji wa kiambajengo kilichotokea mwanzoni mwa sentensi ili kuondoa uradidi.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kielezi

Katika lugha ya Kiswahili, kielezi hutokea baada ya kitenzi, kivumishi au kielezi kingine (Msanjila, 2018; Kihore na wenzake, 2012). Katika utafiti unaoripotiwa katika makala hii, ilibainika kuwa kirai kihusishi hutokea baada ya kielezi husika kwa lengo kutoa taarifa zaidi kuhusu kielezi kilichotangulia. Kutokana na maelezo hayo, kirai kihusishi kinachotokea

baada ya kielezi ni kiambajengo cha hiari kwa sababu kinaweza kuondolewa katika sentensi bila kuathiri maana ya msingi ya sentensi husika. Sambamba na hayo, kirai kihusishi cha baada ya kielezi huweza kutokea baada ya kitenzi au kabla ya kitenzi. Mifano katika Data Na. 8 inadhihirisha haya.

(8) a. Nilitembea **harakaharaka** kutoka mahali hapo (uk. 7).
E KH
b. …nilisikia kamasi likishuka **chini** kama tonge la kichoyo (uk. 28).
E KH
c. Nimeishi **hapa** kwa muda wa miaka mingi (uk 35).
E KH
d. … nilishangazwa **sana** na ukimya wa mazingira hayo (uk. 2).
E KH
e. Mto huu utakapofurika **kabisa** hadi mjini (uk. 12)
E KH
f. Nilihisi ninasukumwa **nje** kwa nguvu (uk. 5).
E KH

Chanzo: *Nagona* (2011)

Viambajengo vilivyopigiwa mistari katika mifano iliyopo katika namba namba 8(a)-(f) ni virai vihusishi vilivyotokea baada ya kielezi. Aidha, virai vihusishi hivyo ni viambajengo vya hiari kwa sababu huweza kuondolewa katika sentensi bila kuathiri maana ya msingi ya sentensi husika. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kielezi hutokana na mfuatano wa viambajengo katika sentensi za Kiswahili kama inavyojitokeza katika Kielelezo Na. 8.

Kielelezo Na. 8: Kirai Kihusishi baada ya Kielezi katika Tungo za Kiswahili



a. harakaharaka	**kutoka**	mahali hapo
b. chini	**kama**	tonge la kichoyo
c. hapa	**kwa**	muda wa miaka mingi
d. sana	**na**	ukimya wa mazingira hayo
e. kabisa	**hadi**	mjini
f. nje	**kwa**	nguvu

Kielelezo Na. 8 kinaonesha kirai kihusishi kinachotokea baada ya kielezi. Katika kielelezo hicho, kirai kihusishi na kielezi huunda kirai kielezi katika lugha ya Kiswahili. Aidha, baada ya kihusishi, kuna kirai nomino kinachotokea kama kiambajengo umbu cha kirai kihusishi. Sambamba na matokeo haya, utafiti wa Wahome (2024) umebaini kuwa, katika lugha ya Kikuyu, kielezi kinachotokea baada ya kitenzi au kivumishi huweza kufuatwa na kirai kihusishi.

Utokeaji wa kirai kihusishi baada ya kihusishi

Kwa mujibu wa Philipo & Kuyenga (2018), kihusishi ni kategoria ya kiuamilifu ambayo huonesha uhusiano wa kategoria zenye hadhi tofauti katika tungo. Mara nyingi, katika lugha ya Kiswahili, vihusishi havipokei viambishi vyovyote, yaani hutokea kama neno huru lisilo na viambishi vyovyote (Mgullu, 1999). Maandiko ya awali (kama vile ya Habwe & Karanja, 2004; Matinde, 2012) yamevibainisha vihusishi kama vivumishi

vya a-unganifu au viwakilishi vya a-unganifu kutokana na kutokea katika nafasi ambazo vivumishi au viwakilishi hutokea. Hata hivyo, utafiti unaoripotiwa katika makala hii umebaini kuwa kirai kihusishi hutokea kwa kufuatana na kihusishi kama inavyodhihirika Data Na. 9[6].

(9) a. Ishara itakapotokea uifuate **hadi** kwenye kitovu cha duara (uk. 16).
H KH

b. kichaa **kutoka** kwenye sayari isiyojulikana alikusudiwa (uk. 36).
H KH

c. Kiumbe hiki kilitembea polepole **hadi** kwenye kiti (uk. 59).
H KH

d. …msichana alituongoza **hadi** kwenye stoo ya majembe (uk. 56).
H KH

Chanzo: *Nagona* (2011)

Katika Data Na. 9(a)-(e), maneno yaliyokozwa ni vihusishi. Baada ya maneno hayo, kuna virai vihusishi ambavyo vimepigiwa mistari. Kulingana na matokeo yaliyozaa utafiti huu, vihusishi viwili vinaweza kufuatana katika tungo za Kiswahili. Aidha, vihusishi hivyo huunda kirai kihusishi ambacho huweza kutokea kwa kukunjiwa katika viambajengo vingine vya kimuundo. Kwa kuzingatia Mkabala wa Kileksika, utokeaji wa kategoria za kimuundo katika lugha mbalimbali hutokana na mfuatano na kategoria zingine katika sentensi. Kwa hiyo, katika sentensi za Kiswahili, kirai kihusishi hutokea baada ya kihusishi kingine kama inavyodhihirika katika Kielelezo Na. 9.

[6] Katika Data Na. 9, maneno ‘hadi’ na ‘kutoka’ yametajwa kama vihusishi kwa kuzingatia kigezo cha kidhima. Maneno tajwa yana dhima ya kuonesha uhusiano baina ya pande mbili za sentensi. Maelezo haya yalifunganama na ufafauzi wa msailiwa mmoja aliyezingatia mbinu ya mfuatano wa maneno katika uainishaji wa maneno tajwa.

Kielelezo Na. 9: Kirai Kihusishi Baada ya Kihusishi katika Tungo za Kiswahili



Katika Kielelezo Na. 9, kirai kihusishi kimetokea baada ya kihusishi. Aidha, viambajengo hivi, kirai kihusishi na kihusishi, huungana na kuunda kirai kihusishi ambacho hutokea katika mazingira mengine ya sentensi. Fikra hizi zinafungamana na za Gitonga & Nandelenga (2022) katika lugha ya Kigembe. Wanabainisha kuwa, katika muundo wa kirai kihusishi katika lugha hiyo, kirai hicho kinaweza kuundwa kwa mfuatano wa vihusishi viwili pamoja na kirai nomino.

Hitimisho

Makala hii imeshughulikia mgogoro wa kimtazamo, miongoni mwa wanasarufi wa lugha ya Kiswahili, kuhusu mawanda na mazingira ya utokeaji wa kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili. Kuna mawanda matatu yaliyotajwa: Kngo+H, Kngo+H+Kngo na H+Kngo. Msimamo wa makala hii ni katika mawanda ya H+Kngo kwa sababu mawanda haya ndiyo yanayoakisi mawanda ya virai vingine vya Kiswahili. Kwa kuzingatia mawanda ya H+Kngo, kirai kihusishi katika sentensi za Kiswahili hutokea baada ya kategoria nane tofauti, yaani baada ya nomino, kitenzi, kivumishi,

kibainishi, kielezi, kiunganishi, kihusishi au kiwakilishi. Hivyo, imebainika kuwa kirai kihusishi ni kirai pekee, miongoni mwa virai vya Kiswahili, kinachotokea baada ya kategoria nyingi za kileksika. Kwa hiyo, usahihi wa utambuzi na ubainishaji wa kirai hiki unatoa uwezekano wa uainishaji wa viambajengo vingine vya sentensi kwa usahihi. Hivyo, umakini unahitajika katika kuainisha kirai hiki katika tungo kwa sababu baadhi ya maneno yanayounda kirai hiki huingiliana na aina zingine za maneno.

Makala hii haikuweza kushughulikia mambo yote kuhusu kirai kihusishi cha Kiswahili. Kwa hiyo, tafiti zingine zinaweza kushughulikia masuala mengine ya kiambajengo hiki ambacho hakijachunguzwa vizuri katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Miongoni mwayo ni: Mosi, utafiti unaweza kuchunguza vigezo vya utambuzi wa kirai kihusishi katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Utafiti huo utaonesha viashiria vinavyoweza kutumika kubainisha kirai kihusishi katika tungo kwa kukitofautisha na virai vingine. Pili, utafiti unaweza kulinganisha au kulinganua muundo na dhima kati ya kirai kuhusishi na kirai kiunganishi au kirai kivumishi katika lugha ya Kiswahili au lugha zingine za Kibantu. Tatu, utafiti unaweza kuchunguza ukubalifu wa sentensi za Kiswahili zinazoanza na virai vihusishi. Katika sarufi ya Kiswahili, sentensi hizo zipo lakini bado hazijafanyiwa utafiti wa kina tofauti na wanasarufi mapokeo wanaozichukulia kuwa hazikubaliki kimuundo.

Marejeleo

Angouri, J. (2010). Quantitative, Qualitative or Both? Combining Methods in Linguistic Research. Katika L. Litosseliti. *Research Methods in Linguistics* (kur. 29-48). London/New York: Continuum International Publishing Group.

Champunga, S.I. (2019). *Muundo na Dhima za Vibainishi Vionyeshi katika Kiswahili Sanifu* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Gimenez, J.C. (2010). Narrative Analysis in Linguistic Research. Katika L. Litosseliti. *Research Methods in Linguistics* (kur. 198-216). London/New York: Continuum International Publishing Group.

Gitonga, J. & Nandelenga, H. (2022). Minimalist Analysis of the Syntactic Structure of the Prepositional Phrase in Kiĩgembe. *GPH-International Journal of Social Science and Humanities Research*, *5*(4), 30-43.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Ilori, F. (2015). Prepositions in Igálà. *Ihafa: A Journal of African Studies*, *7*(1), 139-160.

Kezilahabi, E. (2011). *Nagona*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Khamis, A.M. & J.G. Kiango (2002). *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y.M. (2018). Hadhi na Dhima ya Viunganishi katika Miundo ya Kiswahili. *Mulika*, 25(1), 9-19.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. & Msanjila, Y.P. (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo* (Chapa ya Sita). Dar es Salaam: TUKI.

Lewis, M. (1993). *The Lexical Approach: State of ELT and a Way Forward*. Hove: Language Teaching Publications.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. & Hokororo, J.I. (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo* (Chapa ya Nne). Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A.K. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Lugha ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Mathonsi, N. (2001). Prepositional and Adverb Phrase in Zulu: A Linguistic and Lexicographic Problem. *South African Journal of African Languages*, *21*(2),163-175.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia kwa Sekondari*: Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longman.

Msanjila, Y.P. (2018). Matatizo ya Uainishaji wa Vielezi katika Kiswahili. *Mulika*, 25(1), 20-29.

Ndumiwe, E.J. (2020). *Kurunzi ya Isimu na Muundo wa Kiswahili.* Mwanza: Tridax Africa Company Limited.

Ndumiwe, E.J. (2021). *Mofolojia ya Maneno ya Kiswahili: Upambanuzi wa Kiumbo na Kimuundo*. Mwanza: Tridax Africa Company Limited.

Philipo, Z.T. (2012). Tofauti baina ya Vivumishi na Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 13(1), 125-143.

Philipo, Z.T. & Kuyenga, F.E. (2018). *Sintaksia ya Kiswahili: Nadharia za Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Printers Ltd.

Rubanza, Y.I. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Saluhaya, M.C. (2016). *Kiswahili: Nadharia ya Lugha Kidato cha Tano, Sita na Elimu ya Juu* (Toleo la 2). Dar es Salaam: STC Publishers.

Wahome, J.M. (2024). Syntactic Structure and Role of Prepostional Phrases in Kikuyu Language (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Semarang, Central Java.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI.